# Maombolezo

## 1

* 1 Tazama jinsi mji ulivyoachwa ukiwa,
mji ambao zamani ulikuwa umejaa watu!
Jinsi umekuwa kama mama mjane,
ambaye wakati fulani alikuwa maarufu miongoni mwa mataifa!
Yule aliyekuwa malkia miongoni mwa majimbo
sasa amekuwa mtumwa.

2 Kwa uchungu, hulia sana usiku,
machozi yapo kwenye mashavu yake.
Miongoni mwa wapenzi wake wote
hakuna yeyote wa kumfariji.
Rafiki zake wote wamemsaliti,
wamekuwa adui zake.

3 Baada ya mateso na kufanyishwa kazi kikatili,
Yuda ameenda uhamishoni.
Anakaa miongoni mwa mataifa,
hapati mahali pa kupumzika.
Wote ambao wanamsaka wamemkamata
katikati ya dhiki yake.

4 Barabara zielekeazo Sayuni zaomboleza,
kwa kuwa hakuna yeyote anayekuja
kwenye sikukuu zake zilizoamriwa.

* **1:** Sura hii imetungwa kila beti likianzia, na pia kila mstari katika lile beti, na herufi ya alfabeti ya Kiebrania zikifuatana tangu Aleph (A) hadi Taw (T); zote ni 22.

Malango yake yote yamekuwa ukiwa,
makuhani wake wanalia kwa uchungu,
wanawali wake wanahuzunika,
naye yuko katika uchungu wa maumivu makuu.

5 Adui zake wamekuwa mabwana zake,
watesi wake wana amani.
Mwenyezi Mungu amemletea huzuni
kwa sababu ya dhambi zake nyingi.
Watoto wake wameenda uhamishoni,
wamekuwa mateka mbele ya adui.

6 Fahari zilizokuwa zake zimeondoka
kutoka kwa Binti Sayuni.
Wakuu wake wako kama ayala
ambaye hapati malisho,
wakiwa dhaifu wamekimbia
mbele ya aliyewakimbiza.

7 Katika siku za mateso yake na kutangatanga,
Yerusalemu hukumbuka hazina zote
ambazo zilikuwa zake siku za kale.
Watu wake walipoanguka katika mikono ya adui,
hapatakuwa na yeyote wa kumsaidia.
Watesi wake walimtazama
na kumcheka katika maangamizi yake.

8 Yerusalemu ametenda dhambi sana
kwa hiyo amekuwa najisi.
Wote waliomheshimu wanamdharau,
kwa maana wameuona uchi wake.
Yeye mwenyewe anapiga kite
na kugeukia mbali.

9 Uchafu wake umegandamana na nguo zake;
hakuwaza juu ya maisha yake ya baadaye.
Anguko lake lilikuwa la kushangaza,
hapakuwa na yeyote wa kumfariji.
“Tazama, Ee Mwenyezi Mungu, teso langu,
kwa maana adui ameshinda.”

10 Adui ametia mikono
juu ya hazina zake zote,
aliona mataifa ya kipagani
wakiingia mahali patakatifu pake,
wale uliowakataza kuingia
kwenye kusanyiko lako.

11 Watu wake wote wanalia kwa uchungu
watafutapo chakula;
wanabadilisha hazina zao kwa chakula
ili waweze kuendelea kuishi.
“Tazama, Ee Mwenyezi Mungu, uangalie;
kwa maana nimedharauliwa.”

12 “Je, si kitu kwenu, ninyi nyote mpitao kando?
Angalieni kote mwone.
Je, kuna maumivu kama maumivu yangu
yale yaliyotiwa juu yangu,
yale Mwenyezi Mungu aliyoyaleta juu yangu
katika siku ya hasira yake kali?

13 “Kutoka juu alipeleka moto,
akaushusha katika mifupa yangu.
Aliitandia wavu miguu yangu
na akanirudisha nyuma.
Akanifanya mkiwa,
na mdhaifu mchana kutwa.

14 “Dhambi zangu zimefungwa kwenye nira,
kwa mikono yake zilifumwa pamoja.
Zimefika shingoni mwangu
na Bwana ameziondoa nguvu zangu.
Amenitia mikononi mwa wale
ambao siwezi kushindana nao.

15 “Bwana amewakataa mashujaa
wote walio kati yangu;
ameagiza jeshi dhidi yangu
kuwaponda vijana wangu.
Katika shinikizo lake la kukamulia zabibu
Bwana amemkanyaga Bikira Binti Yuda.

16 “Hii ndiyo sababu ninalia
na macho yangu yanafurika machozi.
Hakuna yeyote aliye karibu kunifariji,
hakuna yeyote wa kuhuisha roho yangu.
Watoto wangu ni wakiwa
kwa sababu adui ameshinda.”

17 Sayuni ananyoosha mikono yake,
lakini hakuna yeyote wa kumfariji.
Mwenyezi Mungu ametoa amri kwa ajili ya Yakobo
kwamba majirani zake wawe adui zake;
Yerusalemu umekuwa
kitu najisi miongoni mwao.

18 “Mwenyezi Mungu ni mwenye haki,
hata hivyo niliasi dhidi ya amri yake.
Sikilizeni, enyi mataifa yote,
tazameni maumivu yangu.
Wasichana wangu na wavulana wangu

wameenda uhamishoni.

19 “Niliita washirika wangu
lakini walinisaliti.
Makuhani wangu na wazee wangu
waliangamia mjini
walipokuwa wakitafuta chakula
ili waweze kuishi.

20 “Angalia, Ee Mwenyezi Mungu, jinsi nilivyo katika dhiki!
Nina maumivu makali ndani yangu,
nami ninahangaika moyoni mwangu,
kwa kuwa nimekuwa mwasi sana.
Huko nje, upanga unaua watu,
ndani, kipo kifo tu.

21 “Watu wamesikia ninavyolia kwa uchungu,
lakini hakuna yeyote wa kunifariji.
Adui zangu wote wamesikia kuhusu dhiki yangu,
wanafurahia lile ulilolitenda.
Naomba uilete siku uliyoitangaza
ili wawe kama mimi.

22 “Uovu wao wote na uje mbele zako;
uwaadhibu vikali
kama ulivyoniadhibu
kwa sababu ya dhambi zangu zote.
Kulia kwangu kwa uchungu ni kwingi
na moyo wangu umedhoofika.”

# 2

* 1 Tazama jinsi Bwana alivyomfunika Binti Sayuni
kwa wingu la hasira yake!
Ameitupa chini fahari ya Israeli
kutoka mbinguni hadi duniani,
hakukumbuka kiti chake cha kuwekea miguu
katika siku ya hasira yake.

2 Bila huruma Bwana ameyameza
makao yote ya Yakobo;
katika ghadhabu yake amebomoa
ngome za Binti Yuda.
Ameuangusha ufalme wake na wakuu wake
chini kwa aibu.

3 Katika hasira kali amevunja
kila pembe† ya Israeli.
Ameuondoa mkono wake wa kuume
alipokaribia adui.
Amemteketeza Yakobo kama moto uwakao
ule uteketezao kila kitu kinachouzunguka.

4 Ameupinda upinde wake kama adui,
mkono wake wa kuume uko tayari.
Kama vile adui amewaua
wote waliokuwa wanapendeza jicho,
amemwaga ghadhabu yake kama moto
juu ya hema la Binti Sayuni.

---

* **2:** Sura hii imetungwa kila beti likianzia, na pia kila mstari katika lile beti, na herufi ya alfabeti ya Kiebrania zikifuatana tangu Aleph (A) hadi Taw (T); zote ni 22. † **2:3** pembe inawakilisha nguvu; pia 2:17

5 Bwana ni kama adui;
amemmeza Israeli.
Ameyameza majumba yake yote ya kifalme
na kuangamiza ngome zake.
Ameongeza huzuni na maombolezo
kwa Binti Yuda.

6 Ameharibu maskani yake kama bustani,
ameharibu mahali pake pa mkutano.
Mwenyezi Mungu amemfanya Sayuni kusahau
sikukuu zake zilizoamriwa na Sabato zake;
katika hasira yake kali amewadharau
mfalme na kuhani.

7 Bwana amekataa madhabahu yake
na kuacha mahali patakatifu pake.
Amemkabidhi adui kuta
za majumba yake ya kifalme;
wameshangilia katika nyumba ya Mwenyezi Mungu
kama katika siku ya sikukuu iliyoamriwa.

8 Mwenyezi Mungu alikusudia kuangusha
ukuta uliomzunguka Binti Sayuni.
Ameinyoosha kamba ya kupimia
na hakuuzuia mkono wake usiangamize.
Alifanya maboma na kuta ziomboleze,
vyote vikaharibika pamoja.

9 Malango yake yamezama ardhini,
makomeo yake ameyavunja na kuyaharibu.
Mfalme wake na wakuu wake wamepelekwa uhamishoni
miongoni mwa mataifa,

sheria haipo tena,
na manabii wake hawapati tena
maono kutoka kwa Mwenyezi Mungu.

10 Wazee wa Binti Sayuni
wanaketi chini kimya,
wamenyunyiza mavumbi kwenye vichwa vyao
na kuvaa gunia.
Wanawali wa Yerusalemu
wameinamisha vichwa vyao hadi chini.

11 Macho yangu yamedhoofika kwa kulia,
nina maumivu makali ndani,
moyo wangu umemiminwa ardhini
kwa sababu watu wangu wameangamizwa,
kwa sababu watoto na wanyonyao wanazimia
kwenye barabara za mji.

12 Wanawaambia mama zao,
"Wapi mkate na divai?"
wazimiapo kama watu waliojeruhiwa
katika barabara za mji,
maisha yao yadhoofikavyo
mikononi mwa mama zao.

13 Ninaweza kusema nini kwa ajili yako?
Nikulinganishe na nini,
ee Binti Yerusalemu?
Nitakufananisha na nini,
ili nipate kukufariji,
ee Bikira Binti Sayuni?
Jeraha lako lina kina kama bahari.
Ni nani awezaye kukuponya?

14 Maono ya manabii wako
yalikuwa ya uongo na yasiyofaa kitu,
hawakuifunua dhambi yako
ili kukuzuilia kwenda utumwani.
Maneno waliyokupa
yalikuwa ya uongo na ya kupotosha.

15 Wote wapitiao njia yako
wanakupigia makofi,
wanakudhihaki na kutikisa vichwa vyao
kwa Binti Yerusalemu:
“Huu ndio ule mji ulioitwa
mkamilifu wa uzuri,
furaha ya dunia yote?”

16 Adui zako wote wanapanua
vinywa vyao dhidi yako,
wanadhihaki na kusaga meno yao
na kusema, “Tumemmeza.
Hii ndiyo siku tuliyoingojea,
tumeishi na kuiona.”

17 Mwenyezi Mungu amefanya lile alilolipanga;
ametimiza neno lake
aliloliamuru siku za kale.
Amekuangusha bila huruma,
amewaacha adui wakusimange,
ametukuza pembe ya adui yako.

18 Mioyo ya watu
inamlilia Bwana.
Ee ukuta wa Binti Sayuni,
machozi yako na yatiririke kama mto
usiku na mchana;

usijipe nafuu,
macho yako yasipumzike.

19 Inuka, lia usiku,
zamu za usiku zianzapo;
mimina moyo wako kama maji
mbele za Bwana.
Mwinulie yeye mikono yako
kwa ajili ya maisha ya watoto wako,
ambao wanazimia kwa njaa
kwenye kila mwanzo wa barabara.

20 “Tazama, Ee Mwenyezi Mungu, ufikirie:
Ni nani ambaye umepata kumtendea namna hii?
Je, wanawake wale wazao wao,
watoto waliowalea?
Je, kuhani na nabii auawe
mahali patakatifu pa Bwana?

21 “Vijana na wazee hujilaza pamoja
katika mavumbi ya barabarani,
wasichana wangu na wavulana wangu
wameanguka kwa upanga.
Umewaua katika siku ya hasira yako,
umewachinja bila huruma.

22 “Kama ulivyoita siku ya karamu,
ndivyo ulivyoagiza mapigo dhidi yangu kila upande.
Katika siku ya hasira ya Mwenyezi Mungu
hakuna yeyote aliyekwepa au kupona;
wale niliowatunza na kuwalea,

adui yangu amewaangamiza.”

# 3

* 1 Mimi ndiye mtu aliyeona mateso
kwa fimbo ya ghadhabu yake.
2 Amenifukuzia mbali na kunifanya nitembee
gizani wala si katika nuru;
3 hakika, amegeuza mkono wake dhidi yangu
tena na tena, mchana kutwa.

4 Amefanya ngozi yangu na nyama yangu kuchakaa
na ameivunja mifupa yangu.
5 Amenizingira na kunizunguka
kwa uchungu na taabu.
6 Amenifanya niishi gizani
kama wale waliokufa.

7 Amenizungushia ukuta ili nisiweze kutoroka,
amenifunga kwa minyororo mizito.
8 Hata ninapoita au kulia ili kuomba msaada,
anakataa kupokea maombi yangu.
9 Ameizuia njia yangu kwa mapande ya mawe,
amepotosha njia zangu.

10 Kama dubu aviziaye,
kama simba mafichoni,
11 ameniburuta kutoka njiani,

* **3:** Sura hii imetungwa kila beti likianzia, na pia kila mstari katika lile beti, na herufi ya alfabeti ya Kiebrania zikifuatana tangu Aleph (A) hadi Taw (T); zote ni 22.

akanirarua na kuniacha bila msaada.
12 Amevuta upinde wake
na kunifanya mimi niwe lengo kwa ajili ya mishale yake.

13 Alinichoma moyo wangu kwa mishale
iliyotoka kwenye podo lake.
14 Nimekuwa kichekesho kwa watu wangu wote,
wananidhihaki kwa wimbo mchana kutwa.
15 Amenijaza kwa majani machungu
na kunishibisha kwa nyongo.

16 Amevunja meno yangu kwa changarawe,
amenikanyagia mavumbini.
17 Amani yangu imeondolewa,
nimesahau kufanikiwa ni nini.
18 Kwa hiyo nasema, “Fahari yangu imeondoka
na yale yote niliyokuwa nimetarajia kutoka kwa Mwenyezi Mungu.”

19 Nayakumbuka mateso yangu na kutangatanga kwangu,
uchungu na nyongo.
20 Ninayakumbuka vyema,
nayo nafsi yangu imezimia ndani yangu.
21 Hata hivyo najikumbusha neno hili
na kwa hiyo ninalo tumaini.

22 Kwa sababu ya upendo mkuu wa Mwenyezi Mungu, hatuangamii,
kwa kuwa huruma zake hazikomi kamwe.
23 Ni mpya kila asubuhi,
uaminifu wako ni mkuu.

24 Nimeiambia nafsi yangu, “Mwenyezi Mungu ni fungu langu,
kwa hiyo nitamngojea.”

25 Mwenyezi Mungu ni mwema kwa wale wanaomtumaini,
na kwa yule anayemtafuta;
26 ni vyema kungojea kwa utulivu
kwa ajili ya wokovu wa Mwenyezi Mungu.
27 Ni vyema mtu kuchukua nira
bado angali kijana.

28 Na akae peke yake awe kimya,
kwa maana Mwenyezi Mungu ameiweka juu yake.
29 Hata azike uso wake mavumbini
bado tumaini litakuwepo.
30 Na atoe shavu lake kwa yule ampigaye,
na ajazwe na aibu.

31 Kwa kuwa watu hawakatiliwi mbali
na Bwana milele.
32 Ingawa huleta huzuni, ataonesha huruma,
kwa kuwa upendo wake usiokoma ni mkuu.
33 Kwa maana hapendi kuwaletea mateso
au huzuni watoto wa wanadamu.

34 Kuwaponda chini ya nyayo
wafungwa wote katika nchi,
35 Kumnyima mtu haki zake
mbele za Aliye Juu Sana,
36 kumnyima mtu haki:
Je, Bwana asione mambo kama haya?

37 Nani awezaye kusema nalo likatendeka
kama Bwana hajaamuru?
38 Je, si ni kwenye kinywa cha Aliye Juu Sana
ndiko yatokako maafa na mambo mema?
39 Je, mwanadamu yeyote aliye hai aweza kulalamika
wakati anapoadhibiwa kwa ajili ya dhambi zake?

40 Tuzichunguze njia zetu na kuzijaribu,
na tumrudie Mwenyezi Mungu.
41 Tuinue mioyo yetu pamoja na mikono yetu
kwa Mungu mbinguni, na tuseme:
42 "Tumetenda dhambi na kuasi
nawe hujasamehe.

43 "Umejifunika mwenyewe kwa hasira na kutufuatilia;
umetuchinja bila huruma.
44 Unajifunika mwenyewe kwa wingu,
ili pasiwe na ombi
litakaloweza kupenya.
45 Umetufanya takataka na uchafu
miongoni mwa mataifa.

46 "Adui zetu wote wamefumbua vinywa vyao
wazi dhidi yetu.
47 Tumeteseka kwa hofu kuu na shida ya ghafula,
uharibifu na maangamizi."
48 Vijito vya machozi vinatiririka kutoka machoni mwangu,
kwa sababu watu wangu wameangamizwa.

49 Macho yangu yatatiririka machozi bila kukoma,
bila kupata nafuu,
50 hadi Mwenyezi Mungu atazame chini
kutoka mbinguni na kuona.
51 Lile ninaloliona huniletea huzuni nafsini
kwa sababu ya wanawake wote wa mji wangu.

52 Wale waliokuwa adui zangu bila sababu
wameniwinda kama ndege.
53 Walijaribu kukomesha maisha yangu ndani ya shimo
na kunitupia mawe;
54 maji yalifunika juu ya kichwa changu,
nami nikafikiri nilikuwa karibu
kukatiliwa mbali.

55 Nililiitia jina lako, Ee Mwenyezi Mungu,
kutoka vina vya shimo.
56 Ulisikia ombi langu: "Usikizibie masikio yako
kilio changu nikuombapo msaada."
57 Ulikuja karibu nilipokuita,
nawe ukasema, "Usiogope."

58 Ee Bwana, ulichukua shauri langu,
ukaukomboa uhai wangu.
59 Umeona, Ee Mwenyezi Mungu, ubaya niliotendewa.
Tetea shauri langu!
60 Umeona kina cha kisasi chao,
mashauri yao yote mabaya dhidi yangu.

61 Ee Mwenyezi Mungu, umesikia matukano yao,

mashauri yao yote mabaya dhidi yangu:
62 kile adui zangu wanachonong'ona na kunung'unikia
dhidi yangu mchana kutwa.
63 Watazame! Wakiwa wameketi au wamesimama,
wananidhihaki katika nyimbo zao.

64 Uwalipe kile wanachostahili, Ee Mwenyezi Mungu,
kwa yale ambayo mikono yao imetenda.
65 Weka pazia juu ya mioyo yao,
laana yako na iwe juu yao!
66 Wafuatilie katika hasira na uwaangamize
chini ya mbingu za Mwenyezi Mungu.

# 4

* 1 Jinsi dhahabu ilivyopoteza mng'ao wake,
dhahabu iliyo safi haing'ai!
Vito vya thamani vimetawanywa
kwenye mwanzo wa kila barabara.

2 Wana wa Sayuni wenye thamani,
ambao mwanzo uzito wa thamani yao
ulikuwa wa dhahabu,
sasa wanaangaliwa kama vyungu vya udongo,
kazi ya mikono ya mfinyanzi!

* **4:** Sura hii imetungwa kila beti likianzia, na pia kila mstari katika lile beti, na herufi ya alfabeti ya Kiebrania zikifuatana tangu Aleph (A) hadi Taw (T); zote ni 22.

3 Hata mbweha hutoa matiti yao
kunyonyesha watoto wao,
lakini watu wangu wamekuwa wasio na huruma
kama mbuni jangwani.

4 Kwa sababu ya kiu ulimi wa mtoto mchanga
umegandamana na kaakaa la kinywa chake,
watoto huomba mkate,
lakini hakuna yeyote awapaye.

5 Wale waliokula vyakula vya kifahari
ni maskini barabarani.
Wale waliokuzwa wakivaa nguo za zambarau
sasa wanalalia majivu.

6 Adhabu ya watu wangu
ni kubwa kuliko ile ya Sodoma,
ambayo ilipinduliwa ghafula
wala hapakuwa na mkono wa msaada.

7 Wakuu wao walikuwa wameng'aa kuliko theluji
na weupe kuliko maziwa,
miili yao ilikuwa myekundu kuliko marijani,
kuonekana kwao kama yakuti samawi.

8 Lakini sasa ni weusi kuliko masizi;
hawatambulikani barabarani.
Ngozi yao imeshikamana juu ya mifupa yao,
imekuwa mikavu kama fimbo.

9 Wale waliouawa kwa upanga ni bora
kuliko wale wanaokufa njaa;
wanateseka kwa njaa, wanatokomea

kwa kukosa chakula kutoka shambani.

10 Kwa mikono yao wenyewe wanawake wenye huruma
wanapika watoto wao wenyewe,
waliokuwa chakula chao
watu wangu walipoangamizwa.

11 Mwenyezi Mungu ametoa nafasi kamilifu ya ghadhabu yake;
ameimwaga hasira yake kali.
Amewasha moto katika Sayuni
ambao umeteketeza misingi yake.

12 Wafalme wa dunia hawakuamini,
wala mtu yeyote wa duniani,
kwamba adui na watesi wangeweza kuingia
kwenye malango ya Yerusalemu.

13 Lakini hili lilitokea kwa sababu ya dhambi za manabii wake,
na maovu ya makuhani wake,
waliomwaga ndani yake
damu ya wenye haki.

14 Sasa wanapapasa papasa barabarani
kama watu ambao ni vipofu.
Wamenajisiwa kabisa kwa damu,
hata hakuna anayethubutu kugusa mavazi yao.

15 Watu wanawapigia kelele, “Ondokeni! Ninyi ni najisi!
Ondokeni! Ondokeni! Msituguse!”

Wanapokimbia na kutangatanga,
watu miongoni mwa mataifa wanasema,
“Hawawezi kukaa hapa zaidi.”

16 Mwenyezi Mungu mwenyewe amewatawanya;
hawaangalii tena.
Makuhani hawaoneshwi heshima,
wazee hawakubaliki.

17 Zaidi ya hayo, macho yetu yalichoka,
kwa kutazamia bure msaada;
tuliangalia kutoka minara yetu
kwa taifa lisiloweza kutuokoa.

18 Watu walituvizia katika kila hatua
hata hatukuweza kutembea katika barabara zetu.
Mwisho wetu ulikuwa karibu, siku zetu zilikuwa zimetimia,
kwa maana mwisho wetu ulikuwa umefika.

19 Waliotufuatia walikuwa wepesi
kuliko tai angani;
walitusaka juu milimani
na kutuvizia jangwani.

20 Mpakwa mafuta wa Mwenyezi Mungu, pumzi ya uhai wetu hasa,
alinaswa katika mitego yao.
Tulifikiri kwamba chini ya kivuli chake
tungeishi miongoni mwa mataifa.

21 Shangilia na ufurahi, ee Binti Edomu,
wewe unayeishi nchi ya Usi.

Lakini kwako pia kikombe kitapitishwa,
Utalewa na kuvuliwa nguo ubaki uchi.

22 Ee Binti Sayuni, adhabu yako itaisha,
hatarefusha muda wako wa kukaa uhamishoni.
Lakini, ee Binti Edomu, ataadhibu dhambi yako,
na atafunua uovu wako.

# 5

1 Kumbuka, Ee Mwenyezi Mungu, yaliyotupata,
tazama, nawe uione aibu yetu.
2 Urithi wetu umegeuziwa kwa wageni,
na nyumba zetu kwa wageni.
3 Tumekuwa yatima wasio na baba,
mama zetu wamekuwa kama wajane.
4 Ni lazima tununue maji tunayokunywa,
kuni zetu zapatikana tu kwa kununua.
5 Wanaotufuatilia wapo kwenye visigino vyetu,
tumechoka na hakuna pumziko.
6 Tumejitolea kwa Misri na Ashuru
tupate chakula cha kutosha.
7 Baba zetu walitenda dhambi na hawapo tena,
na sisi tunachukua adhabu yao.
8 Watumwa wanatutawala
na hakuna wa kutuokoa mikononi yao.
9 Tunapata chakula chetu kwa kuhatarisha maisha yetu
kwa sababu ya upanga jangwani.
10 Ngozi yetu ina joto kama tanuru,
kutokana na fadhaa ya njaa.

11 Wanawake wametendwa jeuri katika Sayuni,
na mabikira katika miji ya Yuda.
12 Wakuu wametungikwa juu kwa mikono yao,
wazee hawapewi heshima.
13 Vijana wanataabika kwenye mawe ya kusagia,
wavulana wanayumbayumba chini ya mizigo ya kuni.
14 Wazee wameondoka katika lango la mji,
vijana wameacha kuimba nyimbo zao.
15 Furaha imeondoka mioyoni mwetu,
kucheza kwetu kumegeuka maombolezo.
16 Taji limeanguka kutoka kichwani petu.
Ole wetu, kwa maana tumetenda dhambi!
17 Kwa sababu hiyo, mioyo yetu inazimia,
kwa sababu ya hayo, macho yetu yamefifia,
18 kwa sababu Mlima Sayuni umekaa ukiwa,
na mbweha wanatembea juu yake.

19 Wewe, Ee Mwenyezi Mungu unatawala milele,
kiti chako cha enzi chadumu kizazi hadi kizazi.
20 Kwa nini watusahau siku zote?
Kwa nini umetuacha kwa muda mrefu?
21 Turudishe kwako mwenyewe, Ee Mwenyezi Mungu,
ili tupate kurudi.
Zifanye mpya siku zetu kama siku za kale,
22 isipokuwa uwe umetukataa kabisa
na umetukasirikia pasipo kipimo.

# Biblica® Toleo Wazi Neno: Maandiko Matakatifu
## The Holy Bible in Swahili: Open Neno: Maandiko Matakatifu 2024

copyright © 2018, 2024 Biblica, Inc.

Language: Kiswahili (Swahili)

Contributor: Biblica, Inc.

Biblica® Toleo Wazi Neno: Maandiko Matakatifu™ ONMM™
Hakimiliki © 2018, 2024 na Biblica, Inc.
Biblica® Open Kiswahili Contemporary Scriptures™
Copyright © 2018, 2024 by Biblica, Inc.

**Creative Commons License**

Kazi hii imewezeshwa kupitia idhini ya kundi la the Creative Commons Attribution-ShareAlike 4.0 International License (CC BY-SA). Ili kuona nakala ya idhini hii, angalia kwenye anwani tovuti ya http://creativecommons.org/licenses/by-sa/4.0 au uandike barua kwa Creative Commons, PO Box 1866, Mountain View, CA 94042, USA.

Biblica® ni alama ya biashara iliyosajilishwa na shirika la Biblica, Inc; unahitaji ruhusa ya kimaandiko kutoka kwa Biblica, Inc. ili kutumia alama ya biashara ya Biblica®. Kulingana na makubaliano ya leseni ya CC BY-SA, unaweza kutoa nakala na kusambaza kazi hii bila kuibadilisha kamwe, mradi tu udumishe alama ya biashara ya Biblica®. Ukibadilisha au kufasiri kazi hii, na hivyo ukanyambua kazi tofauti, sharti uondoe alama ya biashara ya Biblica®. Katika kazi uliyonyambua, sharti uarifu mabadiliko yako, na kutambua kazi yako hivi: “Kazi ya asili ya Biblica, Inc. inapatikana bila bei katika tovuti zawww.biblica.com na open.bible.” Ilani ya hakimiliki sharti iwe katika ukurasa wa kichwa au wa hakilimiliki kama ifuatavyo:

Biblica® Toleo Wazi Neno: Maandiko Matakatifu™ ONMM™
Hakimiliki © 2018, 2024 na Biblica, Inc.
Biblica® Open Kiswahili Contemporary Scriptures™
Copyright © 2018, 2024 by Biblica, Inc.

“Biblica” ni alama ya biashara iliyosajiliwa katika United States Patent and Trademark Office (ofisi ya hataza na alama za biashara Marekani) na shirika la Biblica, Inc. Imetumiwa na ruhusa.

“Biblica” is a trademark registered in the United States Patent and Trademark Office by Biblica, Inc. Used with permission.

Sharti pia uwasilishe kazi uliyonyambua kupitia kwa liseni hiyo hiyo ya CC BY-SA.

Ikiwa ungependa kujulisha Biblica, Inc. kuhusu tafsiri yako ya kazi hii, tafadhali wasiliana nasi katika tovuti https://open.bible/contact-us.

This work is made available under the Creative Commons Attribution-ShareAlike 4.0 International License (CC BY-SA). To view a copy of this license, visit http://creativecommons.org/licenses/by-sa/4.0 or send a letter to Creative Commons, PO Box 1866, Mountain View, CA 94042, USA.

Biblica® is a trademark registered by Biblica, Inc., and use of the Biblica® trademark requires the written permission of Biblica, Inc. Under the terms of the CC BY-SA license, you may copy and redistribute this unmodified work as long as you keep the Biblica® trademark intact. If you modify a copy or translate this work, thereby creating a derivative work, you must remove the Biblica® trademark. On the derivative work, you must indicate what changes you have made and attribute the work as follows: "The original work by Biblica, Inc. is available for free atwww.biblica.com and open.bible."

Notice of copyright must appear on the title or copyright page of the work as follows:

Biblica® Toleo Wazi Neno: Maandiko Matakatifu™ ONMM™

Hakimiliki © 2018, 2024 na Biblica, Inc.

Biblica® Open Kiswahili Contemporary Scriptures™

Copyright © 2018, 2024 by Biblica, Inc.

"Biblica" ni alama ya biashara iliyosajiliwa katika United States Patent and Trademark Office (ofisi ya hataza na alama za biashara Marekani) na shirika la Biblica, Inc. Imetumiwa na ruhusa.

"Biblica" is a trademark registered in the United States Patent and Trademark Office by Biblica, Inc. Used with permission.

You must also make your derivative work available under the same license (CC BY-SA).

If you would like to notify Biblica, Inc. regarding your translation of this work, please contact us at https://open.bible/contact-us.

This translation is made available to you under the terms of the Creative Commons Attribution Share-Alike license 4.0.

You have permission to share and redistribute this Bible translation in any format and to make reasonable revisions and adaptations of this translation, provided that:

You include the above copyright and source information.

If you make any changes to the text, you must indicate that you did so in a way that makes it clear that the original licensor is not necessarily endorsing your changes.

If you redistribute this text, you must distribute your contributions under the same license as the original.

Pictures included with Scriptures and other documents on this site are licensed just for use with those Scriptures and documents. For other uses, please contact the respective copyright owners.

Note that in addition to the rules above, revising and adapting God's Word involves a great responsibility to be true to God's Word. See Revelation 22:18-19.

2025-05-21

---

PDF generated using Haiola and XeLaTeX on 20 May 2025 from source files dated 21 May 2025

72687ba8-7233-577d-bf23-786df16f869d